**TRA SACCOS LIMITED**

# SERA YA RAMBIRAMBI

**Marejeo ya Januari, 2022**

## YALIYOMO


i) Tafsiri ya Maneno. .......... 3

SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI .......... 4

1.1 Sera ya Rambirambi .......... 4

1.2. Dira, Dhamira na Maadili .......... 4

1.2 1. Dira .......... 4

1.2.2. Dhima .......... 4

1.2.3. Maadili ya Msingi .......... 5

SEHEMU YA PILI: MADHUMUNI NA MSINGI WA SERA YA RAMBIRAMBI .......... 6

2.1 Madhumuni ya Sera .......... 6

2.2 Misingi ya Sera .......... 6

2.3 Wigo wa Sera .......... 6

2.4 Marekebisho ya Sera. .......... 7

SEHEMU TA TATU: HUDUMA YA RAMBIRAMBI .......... 8

3.1 Masharti ya Kupata Huduma ya Rambirambi .......... 8

3.1.1 Usajiri wa Mwanachama .......... 8

3.1.2 Uchangiaji wa Huduma .......... 8

3.1.3 Taarifa ya Kifo .......... 8

3.2 Malipo ya Rambirambi .......... 9

SEHEMU YA NNE: MASUALA MBALIMBALI .......... 10

Jedwali Namba 1: Kiwango Cha Mchango na Rambirambi .......... 11

FOMU A: Fomu ya Ujasili .......... 11

i) **Tafsiri ya Maneno.**

1) **Chama**: Chama cha Akiba na Mikopo cha TRA au TRA SACCOS LTD
2) **Rambirambi:** Malipo yanayolipwa kwa mhusika kama mkono wa pole kwa msiba wa mwanachama au mtegemezi wa mwanachama kama ilivyoainishwa katika sera hii.
3) **Mhusika**: Ni mtu atakaye ainishwa kwenye taarifa ya kifo kama mpokeaji wa malipo ya rambirambi
4) **Mtegemezi:** Ni mtu ambaye kifo chake kitapelekea Chama kutoa malipo ya rambirambi kwa mhusika.
5) **Kitambulisho rasmi:** Ni kivuli cha kitambulisho cha Taifa au cha Mpiga kura au Leseni ya udereva pamoja na kibali cha mazishi au cheti cha kifo au taarifa ya kifo kutoka serikali za mtaa pamoja na: (i) Cheti cha kuzaliwa cha Mwanachama ikiwa aliyefariki ni mzazi wa mwanachama (ii) Cheti cha kuzaliwa cha mwenza wa mwanachama na cheti cha ndoa ikiwa aliyefariki ni mkwe wa Mwanachana (iii) Cheti cha ndoa ikiwa aliyefariki ni mwenza wa mwanachama (iv) Cheti cha Kuzaliwa cha mtoto ikiwa aliyefariki ni mtoto wa mwanachama.
6) **Njia rasmi ya mawsiliano**: Anuani ya barua pepe ya Chama ambayo ni info@trasaccos.co.tz
7) **Mwanachama**: Mtu mwenye sifa kama ilivyo ainishwa kwenye kifungu namba 13 cha Masharti ya Chama.
8) **Sera:** Sera ya rambirambi
9) **Meneja**: Mtendaji Mkuu wa Chama

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

TRA SACCOS LTD ni Asasi ndogo ya fedha iliyoanzishwa na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kuwahudumia wanachama wake kwa kuwapatia huduma mbalimbali za kifedha ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi, kijamii na ya kimazingira kwa kufuata taratibu za kidemokrasia, misingi, Kanuni na Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na Masharti ya Chama.

Bodi ya Chama imeendelea kutekeleza jukumu hili kwa ufanisi na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za vyama vya Ushirika, masharti ya Chama na Sera mbalimbali kama zinavyoidhinishwa na Wanachama ili kuhakikisha kwamba Chama kinaendeshwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia taratibu na uwezo wa Chama.

### 1.1 Sera ya Rambirambi

Bodi katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwemo uandaaji na utekelezaji wa Sera mbalimbali kwa lengo la kukiendesha Chama kwa ufanisi na misingi ya Utawala Bora, imeandaa Sera ya Rambirambi ili kuweza kutoa huduma bora na zenye usawa kwa Wanachama.

Sera ya Rambirambi imeandaliwa kwa kuzingatia misingi ya Sheria ya Ushirika, Kanuni za Ushirika pamoja na Masharti ya Chama na mahitaji halisia ya wanachama. Sera hii inalenga kuwezesha na kuleta ufanisi katika kuwahudumia Wanachama kwa ukaribu zaidi popote pale walipo.

### 1.2. Dira, Dhamira na Maadili

#### 1.2 1. Dira

Kuwa chama cha Akiba na Mikopo cha kisasa na Kuigwa Tanzania. Kujenga mfumo madhubuti wenye usawa, uwazi, uwajibikaji na ubora wa kazi katika mfumo mzima wa utoaji, ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo na utoaji wa taarifa ya fedha kwa wakati.

#### 1.2.2. Dhima

Kuinua, kustawisha na kuboresha hali ya Kiuchumi na kijamii kwa Wanachama, kwa kuwahamasisha kuweka akiba na kuwapatia Mikopo yenye Manufaa na riba nafuu

### 1.2.3. Maadili ya Msingi

a) Kutoa huduma nzuri na zenye ufanisi kwa Wanachama kwa Uadilifu, Uaminifu, Haki na Usawa,

b) Kubuni, kuboresha na kuendeleza huduma bora kwa Wanachama,

c) Kutumia utaalamu katika Uongozi na Kufuata misingi ya Utawala bora.

d) Kuendesha Chama kwa weledi na kufuata misingi ya Utawala bora na uwajibikaji na

e) Kushiriki katika majukumu ya kijamii kwa Umoja na Ushirikiano.

## SEHEMU YA PILI

## MADHUMUNI NA MSINGI WA SERA YA RAMBIRAMBI

### 2.1 Madhumuni ya Sera

Sera hii imejengwa kwa nia ya kuandaa njia bora za kuhudumia Wanachama pale wanapofariki au kufiwa na wategemezi wao kama walivyoainishwa katika sera hii.

Madhumuni mengine ya sera ni kama ifuatavyo:

i. Kuwapatia Wanachama huduma Bora

ii. Kuwawezesha Wanachama kukabiliana na matatizo ya msiba yanapotokea.

iii. Kuwajengea wanachama utamaduni wa kusaidiana.

iv. Kujenga mshikamano baina ya Wanachama.

v. Kuweka mwongozo wa namna bora ya kutoa huduma ya Rambirambi kwa Wanachama.

### 2.2 **Misingi ya Sera**

Sera imeandaliwa kwa kuzingatia Sheria na miongozo mbalimbali za nchi na maagizo mengine kama ifuatavyo:-

- Sheria ya Vyama vya Ushirika, na Kanuni za Ushirika.
- Masharti ya Chama
- Mpango Mkakati wa Chama
- Mhitaji ya Wanachama kupitia mijadala na maamuzi ya Mkutano Mkuu

### 2.3 **Wigo wa Sera**

2.3.1 (a) Sera hii itahusisha mwanachama na wategemezi wa mwanachama kama ifuatavyo

1. Wazazi wa Mwanachama
2. Wakwe wa Mwanachama
3. Mwenza wa Mwanachama
4. Watoto wa Mwanachama

(b) Kwa madhumuni ya sera hii, mzazi ni mzazi wa asili (Biological parent) au mtu ambaye mwanachama amemtambulisha kwenye **FOMU A** kama mzazi wake. Mwanachama hatanufaika zaidi ya mara moja katika kila nafasi ya mtegemezi isipokuwa kwa nafasi ya mtoto. Kukiuka kifungu hiki ni kosa linaloweza kupelekea mwanachama kusimamishwa ama kufutiwa uanachama chini ya kifungu cha 17 cha masharti ya chama.

2.3.2 Mwanachama atatakiwa kujaza na kuwasilisha kwenye Chama taarifa za wategemezi wake kwa kujaza **Fomu A** iliyopo kwenye nyongeza ya sera hii.

**2.4 Marekebisho ya Sera.**

Bodi ya Chama inaweza kufanya mapitio na maboresho ya Sera hii mara kwa mara kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Ushirika, maoni na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali, wakiwemo wanachama kupitia vikao vya Matawi au Mkutano Mkuu ili kuleta ufanisi wa utendaji wa shughuli za Chama.

Mapendekezo ya marekebisho ya Sera, yatawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa Wanachama kwa maamuzi kabla ya kuanza kutumika rasmi.

## SEHEMU TA TATU

## HUDUMA YA RAMBIRAMBI

Rambirambi ni moja kati ya huduma zitolewazo kwa kila Mwanachama kwa kuchangia huduma hii kila mwezi.

### 3.1 **Masharti ya Kupata Huduma ya Rambirambi**

#### ***3.1.1*** *Usajiri wa Mwanachama*

(a) Mwanachama atawasilisha kwenye Chama taarifa za wategemezi wake kwa kujaza **Fomu A** iliyopo kwenye nyongeza ya sera hii.

(b) Mwanachama anatakiwa kuhuisha taarifa za wategemezi wake kila mara inapotokea mabadiliko ya wategemezi wake.

#### *3.1.2 Uchangiaji wa Huduma*

a) Kila Mwanachama atachangia kiasi cha fedha kila Mwezi kama ambavyo itakuwa imeamuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama (Angalia Jedwali la 1). Mwanachama atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa michango yake inawasilishwa katika Chama kila mwezi.

b) Mwanachama hatalipwa rambirambi endapo hachangii au anadaiwa limbikizo lolote la mchango kabla ya janga la kifo kutokea.

#### *3.1.3 Taarifa ya Kifo*

Taarifa ya kifo itawasilishwa na Mwenyekiti wa Kituo husika kwa Meneja wa Chama kwa njia rasmi ya mawasiliano. Chama kinaweza kujiridhisha kwa njia mbalimbali juu ya taarifa ya kifo iliyowasilishwa na mwanachama, ikiwemo kuwasiliana na kuomba uthibitisho kutoka Idara ya Rasilimali Watu, Makao Makuu ya TRA.

**Taarifa ya kifo anatakiwa kuwa na taarifa muhimu kama vile:**

● Namba ya ajira na jina kamili la mwanachama au mhusika. Namba ya ajira haitahitajika kwa mhusika asiye mwajiriwa.

● Jina kamili la marehemu na nakala ya kitambulisho rasmi.

● Namba ya simu au akaunti ya benki ya mhusika.

Taarifa zitakazo pokelewa zitasajiliwa katika daftari maalum na kuhakikiwa kabla ya malipo kufanyika.

3.2 Malipo ya Rambirambi

(a) Rambirambi italipwa kwa njia ya simu au benki kwenye namba ya mhusika na kumbukumbu ya malipo kuhifadhiwa kwenye faili husika la Rambirambi. Kwa madhumuni ya kifungu hiki, mhusika ni mtu atakayeainishwa kwenye taarifa ya kifo kuwa ndiye atakayepokea malipo ya rambirambi.

(b) Malipo ya rambirambi yataandaliwa na Idara ya Fedha na kuidhinishwa na Meneja.

## SEHEMU YA NNE

## MASUALA MBALIMBALI

a) Mhusika ahakikishe kuwa anatoa namba sahihi ya mitandao ya simu au akaunti ya benki iliyothibitishwa ambayo ndiyo itatumika kulipa rambirambi hiyo.

b) Taarifa ya kifo iwasilishwe mapema kadiri iwezekanavyo.

c) Malalamiko yote yawasilishwe Makao Makuu ya Chama.

d) Matumizi wa pesa yote itakayopatikana kama makusanyo kutokanana huduma hii ya rambirambi yatatumika kama itakavyoelezwa na sera ya uwekezaji.

**Jedwali Namba 1: Kiwango Cha Mchango na Rambirambi**

| KIASI CHA MCHANGO KILA MWEZI (Tzs) | KIASI CHA RAMBIRAMBI KWA MWANACHAMA NA MWENZA (Tzs) | KIASI CHA RAMBIRAMBI KWA MZAZI, MKWE NA MTOTO (Tzs) |
|---|---|---|
| 10,000 | 2,000,000 | 2,000,000 |

**FOMU A: Fomu ya Ujasili**

Taarifa za Mwanachama na Wategemezi wake

| JINA KAMILI | NAMBA YA UANACHAMA | NAMBA YA SIMU | BARUA PEPE |
|---|---|---|---|
| | | | |

Taarifa za Wategemezi

| MTEGEMEZI | JINA KAMILI |
|---|---|
| Mwenza | |
| Mzazi 1 | |
| Mzazi 2 | |
| Mkwe 1 | |
| Mkwe 2 | |

Mimi………………………………………………. (jina kamili) Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa kwenye Fomu hii ni sahihi na kweli.

Saini……………………………………… Tarehe……………………………

**MAELEKEZO MUHIMU**

**1.** Kwa madhumuni ya sera hii, mzazi ni mzazi wa asili (Biological parent) au mtu ambaye mwanachama amemtambulisha kwenye fomu hii kama mzazi wake.

**2.** Mwanachama hatanufaika zaidi ya mara moja kwa kila nafasi ya mtegemezi isipokuwa kwa nafasi ya mtoto**.** Kukiuka kifungu hiki ni kosa linaloweza kupelekea mwanachama kusimamishwa ama kufutiwa uanachama chini ya kifungu cha 17 cha masharti ya chama.

**TRA SACCOS LTD** **OFISI YA MRAJISI**

____________________________________

Pilly Marwa

Mwenyekiti TRA SACCOS LTD